
# Zaburi 137 - Siku nilipokuita

**Siku ya Mungu ya 17, mwaka C**

Eugène AMPIRE BISIMWA




1. Nitakutukuza, eeBwana, kwamoyo wangu wote,
   Kwani umesikia maneno ya kinywa changu.
   Mbele ya malaika nitakuimbia,
   Nitaliangukia hekalu lako takatifu.

2. Nitatukuza jina lako / kwa ajili ya wema wa uaminifu wako.
   Kwa maana umekuza kuliko yote / jina lako na ahadi yako.
   Siku nilipokuita ulinisikiliza,
   Uliongeza nguvu rohoni mwangu.

3. Bwana yuko juu / lakini anamwangalia mnyonge,
   Na mwenye kiburi anamtambua toka mbali.
   Ninapokwenda kati ya taabu / Wewe unasitawisha uzima wangu.
   Unanyosha mkono wako kuizuia hasira ya adui zangu,

4. Mkono wakowa kuume unanisalimisha;
   Bwana atatimiliza kwangu aliyonitendea.
   Ee Bwana, wema wako ndio wa milele:
   Usiache kazi ya mikono yako.